Maelezo juu ya dawa



ddI (Didanosine, Videx, Videx-EC)

Kwa Nini Nimepewa Dawa Ya ddI?

- ddI (ambayo pia hujulikana kama didanosine, Videx, Videx-EC) ni dawa inayotumika pamoja na mchanganyiko wa dawa nyingine kutibu maambukizi ya vijidudu vya ukimwi.
- ddI husaidia kuzuia protini inayoitwa “reverse transcriptase.” Kutokana na kazi hii, dawa hii huwekwa kwenye kundi la dawa zinazoitwa Reverse Transcriptase Inhibitors (RTIs). Vijidudu vya maambukizi ya ukimwi huhitaji protini hii ili kuzaliana, kwa hiyo kwa kuwa dawa hii huzuia protini hii inasaidia kupunguza nguvu za ugonjwa wa maambukizi ya vijidudu vya ukimwi.
- Matumizi ya dawa hii huweza kupunguza wingi wa vijidudu vya maambukizi mwilini mwako. Pia husaidia kupunguza uwezekano wa kupatwa na magonjwa yanayoendana na ukimwi, na kukuwezesha kuwa na afya njema kwa muda mrefu au kukurudishia afya yako kabisa. Vilevile dawa hii husaidia kupunguza uharibifu wa mfumo wako wa kupigana na magonjwa.

Nitatumiaje Dawa Hii?

- ddI hupatikana kwenye nguvu mbalimbali kwenye mifumo ya vidonge vya kutafuna (Videx) au vidonge vilivyowekwa kwenye vijifuko vidogo - capsules (Videx-EC). Kiwango cha matumizi ya kila mtu hutegemea uzito wa mwili wa mtumiaji.

Canadian AIDS Treatment Information Exchange
Réseau canadien d’info-traitements sida
www.catie.ca

AFRICANS IN PARTNERSHIP AGAINST AIDS
www.apaa.ca

Maamuzi juu ya matibabu ya aina mbalimbali yanahitajika kufanywa kwa kushauriana na mtaalamu aliyehitimu kwenye mambo ya afya na mwenye ujuzi juu ya magonjwa yanayoendana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na matibabu atakayoamuliwa kutumiwa.

- Inapendekezwa kutumia ddI kabla ya kula chakula, lisaa limoja kabla au masaa mawili baada ya kula. Uwepo wa chakula mwilini huzidisha kiwango cha tindikali (acid) tumboni na kuchangia katika kuharibu nguvu ya dawa.
- Unaweza kutumia vidonge vya ddI kwa kutumia moja ya njia tatu tofauti zifuatazo:
- Kwa kutafuna vidonge hadi vinasagika kabisa, kisha kumeza na kunywa maji kidogo ili kusukumiza mabaki yote tumboni. Usimeze kidonge kizima bila kutafuna.
- Kuvisaga vidonge kisha kuvichanganya na maji kwa kiasi cha c.c.30 (vijiko 2 vya chakula) ili kuyeyusha unga wake na kuunywa.
- Kukiyeyusha kidonge kizima kwenye kikombe cha maji na kunywa kikombe kizima cha maji ya mchanganyiko huu katika kipindi cha lisaa limoja.
- Vidonge vya ddI vinaweza kumezwa vikiwa vizima bila kutafunwa au kusagwa.
- Usichanganye ddI na maji ya ladha ya ndimu/limao (citric fruits juices) au vinywaji baridi kama soda (pop), kwani vinywaji hivi mara nyingi vina tindikali ambayo ina uwezo wa kuharibu nguvu za dawa. Unashauriwa kutumia maji au maziwa tu.
- Kumbuka kuswaki meno yako kila baada ya kunywa dawa yako kuepukana na kuoza kwa meno.
- ddI inahitajika kuhifadhiwa kwenye joto la kawaida na mahali pakavu. Jaribu kuhifadhi dawa hii jinsi ilivyokuja ikiwa imewekwa kwenye kikopo chake ulichopewa nacho. Usiweke dawa hii bafuni au jikoni, kwani unyevunyevu huweza haribu dawa hii.
- Hifadhi dawa hii mbali na watoto.

Nifanye Nini Nikisahau Kunywa Vidonge Vyangu?

- Meza dawa zako ulizosahau mapema iwezekanavyo. Ikiwa ni karibu na saa mbili kabla ya muda wa kumeza dawa nyingine, endelea na ratiba yako ya kawaida. Usimeze dawa zako mara mbili ya kiwango utakiwacho ili kulipizia ile uliyosahau.

- Tafiti za kisanyansi zilizofanyika karibuni zimegundua kuwa ili dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi ziweze kufanya kazi vizuri, dawa zote hazina budi kutumiwa mara kwa mara na kwa mfululuzo ilivyoelekezwa. Kuacha au kuruka kumeza dawa zako kunasababisha kupungua kwa nguvu za dawa hizi na kuvifanya vijidudu vya maambukizi kubadilika na kuwa sugu kwa dawa.

Madhara Ya Yaletwayo Na Matumizi ddI Ni Yepi?

- Madhara makuu yatokanayo na matumizi ya ddI ni:
  - Kuwakwa (kama unaungua na moto) na kufa ganzi mikononi na miguuni (neuropathy) Maumivu makali ya tumbo ambayo husambaa hadi mgongoni, na
  - kukuletea kichefuchefu na kutapika (kuvimba kwa kongosho – swallen pancreas gland)
- Madhara mengine ya kawaida yatokanayo na matumizi ya ddI ni kama:
  - Maumivu ya kichwa, kizunguzungu , na kuchanganyikiwa
  - Kuhara au/na kuvimbiwa
  - Kichefuchefu na kutapika
  - Kukosa usingizi
  - Upele wa ngozi
  - Kukaaukwa kwa mdomo, vidonda vya mdomoni au kubadilikwa kwa vionjo vya ulimi
  - Maumivu ya maungo ya mwili
  - Kubadilika kwa kiwango cha blood's uric acid na utendaji ya ini

- Nyakati chache, ddI inaweza kusababisha kupunguwa kwa chembechembe nyeupe za damu mwili mwako (jambo ambalo linaweza sababisha kuongezeka kwa mashambulizi ya vijidudu vya magonjwa), chembechembe ndogo za damu -platelets (zinazosaidia kuganda kwa damu ili kusitisha kutokwa kwa damu kunakoweza kusababishwa na ajali au mkato wowote mwilini kitendo ambacho kinaweza sababisha kutokwa kwa damu nyingi unapatwapo na ajali).
- Madhara haya yatokanayo na matumizi ya ddI yanaweza kupunguzwa na kubadilishwa kama yanagundulika mapema na kuwezesha kusitishwa au kupunguzwa kwa matumizi ya dawa hii. Kama unajisikia dalili hizi, ongea na

daktari au mfamasia wako mapema iwezekanavyo. Usisitishe au kubadilisha dawa zako bila kuongea nao.

Je, Naweza Kutumia ddI Na Dawa Nyingine?

- ddI inaweza kuleta madhara kadhaa ikitumiwa pamoja na dawa nyingine. Ni muhimu kumweleza daktari wako au mfamasia wako juu ya dawa nyingine zote ulizoandikiwa na unazotumia, (ikiwa ni pamoja na vitamini na dawa za mitishamba).
- Unaweza kushauriwa kubadlisha kiwango cha ddI unachotumia kama utakuwa pia unatumia tenofovir (Viread). Ongea na daktari wako kama unatumia dawa hizi kwa pamoja.
- Usitumie ddI pamoja na ddC (Hivid)
- ddI inahitajika kutumiwa masaa mawili kabla au baada ya kutumia Ketoconazole (Nizoral), Cipro (Ciprofloxicin) na Tetracycline, na lisaa limoja kabla au baada kama unatumia delavirdine (Rescriptol) na indinavir (Crixivan).
- Wasiliana na daktari wako kama utakuwa pia unatumia Pentamadine au ganciclovir (Cytovene).

Je Naweza Kutumia ddI Na Pombe Au Dawa Za Mitaani?

- Epukana na unywaji wa pombe kama unatumia ddI. Pombe inaweza zidisha adhari za kuvimba kwa kongosho (swollen pancreas gland).
- ddI huweza kuingiliana kiutendaji na madawa ya mitani. Ongea na daktari wako au mfamasia kama unatumia dawa za mitaani ili waweze kukushauri jinsi ya kujikinga.

Je, Naweza Kutumia ddI Kama Ni Mjamzito Au Nanyonyesha?

- Kama u mjamzito na unataka kutumia ddI, tafadhali pata ushauri kutoka kwa daktari wako.

- Kwa kuwa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi huweza kuambukizwa kwa kunyonyesha, wanawake wenye mambukizi ya vijidudu vya ukimwi hawashauriwi kunyonyesha.

Natakiwa Kujihadhari Vipi Zaidi Ninapotumia ddI?

- Kama una matatizo za figo zako, hakikisha umamweleza daktari wako kabla ya kuanza kutumia ddI.
- Timiza mihadi na daktari wako kwa ajili ya kufanya vipimo vya damu kutazama kama figo zako zinafanya kazi vizuri.
- Hakikisha una dawa za kutosha kuendelea na matibabu yako.
- ddI haiui vijidudu vya maambukizi ya ukimwi au kutibu ukimwi. Pia haizui kusambaa au kuambukiza kwa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi, hivyo tafadhali jaribu kuwa mwangalifu na kutumia kinga zihitajikazo unapotaka kukutana kimwili na mtu mwingine (tumia kondom za latex) au kama unatumia madwa ya kulevya (tumia mabomba na sindano mpya na safi).

Shirika la kubadilishana maelezo juu matibabu ya ukimwi Kanada (The Canadian AIDS Treatment Information Exchange – CATIE) na Shirikisho la waafrika katika kupigana na ukimwi (Africans in Partnership Against AIDS - APAA) kwa nia nzuri kabisa wanatoa maelezo kwa watu wanaoishi na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi/Ukimwi ambao wangependa kutawala afya zao wenyewe kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wanaowapatia matibabu. Hata hivyo, maelezo haya yanayochapishwa au kutolewa na CATIE au APAA hayawezi kuchukuliwa kama ushauri wa kiafya. Hatushauri au kusisitiza juu ya tiba moja juu ya nyingine. Hivyo tunawashauri watumiaji ya maelezo yetu kupitia maelezo ya matibabu mengine yanayotolewa na vyanzo mbalimbali kwa upeo mkubwa iwezekanavyo. Tunawashauri watumiaji wa maelezo haya na kusisitiza kuwa ni muhimu kushauriana na wataalamu ya afya na tiba waliohitimu mafunzo yao kabla ya kuamua, kutumia au kuanza jambo lolote juu ya matibabu.

Vile vile, hatuthibitishi au kudhamini ukweli au ufarisi na ujuzi wa maelezo yanayochapishwa au kupatikana kutoka CATIE au APAA. Watumiaji wanaotumia au kutegemea maelezo haya wanafanya hivyo kwa kuthubutu wenyewe na matokeo yake yakiwa mabaya yatakuwa juu yao. Si CATIE wala APAA, au Wizara ya Afya Kanada, au wafanyakazi wao, wakurugenzi, maafisa au watu wanaojitolea wataweza kuhusishwa na uharibifu wa aina yeyote unaoweza kutokea kwa kutumia vizuri au vibaya maelezo haya. Mawazo na maelezo yaliyotolewa hapa au kwenye nakala yeyote au ilani/tangazo lolote.

Copyright: This Fact Sheet is made available through a collaboration between Africans in Partnership Against AIDS (APAA), Asian Community AIDS Services (ACAS) and the Canadian AIDS Treatment Information Exchange (CATIE). Original content developed by ACAS, 2001. Translation into Swahili and Hausa by APAA, 2004.

This information is also available in Chinese, Tagalog and Vietnamese

Funding has been provided by Health Canada, under the Canadian Strategy on HIV/AIDS

Supported by an unrestricted educational grant from GlaxoSmithKline in partnership with Shire BioChem

www.acas.org